JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

Multisectoral magazine

DECEMBER-JANUARY 2023 | ISSUE NO 005




## BWAWA LA NYERERE MTAJI KWA TAIFA

16 UMUHIMU WA JNHPP

KUTAKUWA NA UMEME WA UHAKIKA NA GHARAMA NAFUU
KUVUTIA WAWEKEZAJI KUWEKEZA NCHINI
UCHUMI WA NCHI UTAKUA KWA KASI
KUPUNGUZA MFUMUKO WA BEI ZA BIDHAA ZA VIWANDA NA KILIMO

TSHS.25,000 KSHS.1,300 USHS 40,000
ISSN 2799-225X | LESENI 00000021
www.tz&beyond.co.tz





# BODI
YA WAHARIRI

**AFISA MTENDAJI MKUU**
Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

**MHARIRI MTENDAJI**
Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA**
Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**
Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

**MWENYEKITI/MLEZI**
Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com

**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com


TZ&BEYOND




18
RAIS SAMIA JNHPP ILINIUMIZA KICHWA



44
Bwawa la Nyerere lafikia asilimia 80.2



24
Mkombozi wa nishati nchini







30
Misri yaacha ujumbe



29
Faida ya ujenzi wa mradi



24
Ukuzaji wa uchumi wa Tanzania



42
Fedha za mradi wa JNHPP zipo



15
Bwawa la umeme lafikia 80.2%



22
Mradi wa pili ni wa kupeleka umeme kwenye migodi



42
Uzalishaji ajira

JICHO LA TZ&BEYOND



MWENYEKITI: DR. THOMAS KASHILILAH

JARIDA: TZ&BEYOND

COVER STORY: BWAWA LA NYERERE

## JNHPP NI ALAMA YA USHINDI KWA TANZANIA

MRADI wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) unaelekea kukamilika, tayari njia ya kwanza ya mradi huo ambayo inachepusha maji ya mto na kuyaingiza kwenye bwawa imekamilika kwa asilimia 100 na tayari imeshazinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan .

Kimsingi mradi huu utakaokuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 2115 za umeme ni alama ya ushindi kwa Tanzania na nchi itaanza kujitosheleza na nishati ya umeme wa maji sanjari na umeme wa gesi na nishati nyengine mbadala.

Ukweli ni kuwa mradi huu una faida nyingi tofauti na hoja lukuki zilizokuwa zikitolewa awali na baadhi ya mashirika ya kitaifa na ya kimataifa.

Ikumbukwe kuwa mradi huu ulipaswa kutekelezwa tangu mwaka 1970 wakati wa uongozi wa awamu ya kwanza iliyokuwa chini ya Hayati Rais Julius Nyerere, ambaye ndie aliasisi wazo la kujenga mradi mkubwa ili kuiondoa nchi kwenye tatizo la umeme, hatua ambayo ingesaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji viwandani na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Wakati Tanzania ikiwa katika harakati za kutafuta ufumbuzi wa tatizo la umeme, mwaka 1982, UNESCO ililingiza pori hilo la akiba la Selous kwenye urithi wa dunia.

Uamuzi huo wa UNESCO ulikuja kipindi ambacho tayari Tanzania ilikuwa imeshaanza mchakato wa kutaka kujenga bwawa hilo.

Pamoja na ukweli huo, UNESCO na WWF walikuwa vinara wa kuupinga mradi huo kwa hoja ya kulinda malikale na ekolojia ya eneo hilo.

WWF na UNESCO ni taasisi zinazoshughulika na masuala ya hifadhi za mazingira, ekolojia, utamaduni na Wanyama pori.

Ingawa Tanzania ilikuwa sahihi, lakini taasisi hizo zilibeba hoja kuwa endapo mradi huo utatekelezwa upo uwezekano wa vyanzo vya maji ndani ya mto Rufiji ambavyo vinatiririsha maji yanayotegemewa na binadamu na wanyama kukauka.

Kwamba hatua hiyo ingeathiri sekta ya utalii, aidha walibeba hoja kuwa samaki hasa aina ya Kambakochi na wengine wanaopatikana katika eneo hilo wangepungua na kuathiri maisha ya wananchi wanaopakana na eneo hilo.

Athari nyengine walioiona ni mradi huo kusababisha mmomonyoko mkubwa wa ardhi ambao ni hatari kwa mazingira ya eneo husika, jambo ambalo limeonekana kukosa mashiko.

Sababu hizo tajwa na ukosefu wa fedha za kugharamia mradi huo zilichangia kutotekelezwa kwa mradi huo kuanzia mwaka 1970 hadi mwaka 2015. Hatimeye mwaka 2017 Jemedari na mwanamapinduzi , Hayati Rais Dkt. John Magufuli alifanya kweli na kuanza kuutekeleza kwa kuujenga kwa awamu moja tofauti na ilivyopendekezwa awali kuujenga kwa awamu zaidi ya mbili.

Uamuzi wa Hayati Rais Mgufuli ulisukumwa na tafiti zilizofanywa na kubainisha kuwa mradi huo ni salama na una faida nyingi kwa Tanzania kama ambavyo Jicho la TZ&BEYOND lilivyoziainisha kwenye andiko hili na maandiko mengine mengi yaliyomo ndani ya jarida hili, lakini pia Shirika la Umeme nchini (TANESCO) limeweka wazi kuwa kukamilika kwa mradi huo kutaleta faida nyingi ikiwemo nchi kuwa na umeme wa ziada na kuondoa mafuriko.

Bei ya umeme itashuka hatua ambayo itachochea zaidi matumizi ya nishati hiyo na kuachana na matumizi ya kuni hivyo kulinda mazingira.

Ujenzi wa bwawa hilo utakapokamilika na kuanza kazi utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2115, hatua hii itasaidia nchi kuwa na umeme mwingi wa ziada hali itakayoongeza ukuaji wa uchumi kwa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja. Aidha mradi huo utasaidia kurahisisha kilimo cha umwagiliaji katika ukubwa wa heka 200,000 hatua itakayowafaidisha wakulima wadogo na wakubwa.

Kutakuwa na uvuvi na ufugaji wa samaki wa uhakika, wanyama wengi watapata maji na hawatasafiri umbali mrefu kusaka maji na malisho ,bei ya umeme itashuka kwa kiwango kikubwa na Wanyama wengi wataonekana kwa urahisi.

Mradi utavutia wawekezaji kwa kuwa na umeme wa uhakika na ndani ya bwawa kutakuwa na visiwa ambapo pia kunaweza kujengwa hoteli za kitalii kutokana na kwamba bwawa hilo litakuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 55,000.

Kuna miradi mingine ya kijamii itajengwa katika vijiji vilivyopo karibu na bwawa hilo mara tu uzalishaji wa umeme utakapokuwa unaendelea.

Jicho la TZ&BEYOND limejulishwa kuwa mradi huu unakadiriwa kutumia Shilingi trilioni 6.5 ambazo ni fedha zetu zinazotokana na kodi za Watanzania ambapo mpaka kufikia Novemba 2022, Serikali imemlipa Mkandarasi Shilingi trilioni 4.5 sawa na 70% ya mradi. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2022, mradi huu umeajiri watu 12,275 ambapo kati ya walioajiriwa, Watanzania ni 11,164 sawa na 90.97%.





# BWAWA LA NYERERE MTAJI KWA TAIFA

TANZANIA imedhamiria kujikwamua kiuchumi ili kuendana na kasi ya maendeleo ya dunia. Dhamira hiyo inaifanya serikali kusaka mbinu na namna sahihi za kufanikisha mipango yake.

**Miongoni mwa harakati hizo ni uanzishwaji wa ujenzi wa mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP) .**

# Bwawa la Nyerere mtaji kwa Taifa

TANZANIA imedhamiria kujikwamua kiuchumi ili kuendana na kasi ya maendeleo ya dunia.

Dhamira hiyo inaifanya serikali kusaka mbinu na namna sahihi za kufanikisha mipango yake.

Miongoni mwa harakati hizo ni uanzishwaji wa ujenzi wa mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP) .

Mradi huu ambao uko katika hatua za kukamilika unatarajia kuzalisha umeme wa Megawati 2,115,.

Kukamilika kwake na kuanza kufanya kazi kusudiwa kutakuwa mtaji mpya utakaosukuma kwa kasi maendeleo ya nchi na wananchi wake.

Ni wazi kasi ya ukuaji wa uchumi itaongezeka, kwani nchi itakuwa na umeme wa uhakika.

Kwa sasa Tanzania inatazamwa kama nchi yenye uchumi unaokuwa kwa kasi kwa ukanda wa Afrika Mashariki, ingawa janga la Corona limerudisha nyuma kasi hiyo kwa kiasi kikubwa .

Historia ya mradi huu inaanzia wakati wa utawala wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, lakini utekelezaji wa sasa unatokana na uamuzi mgumu na wenye kujali maslahi mapana ya Tanzania ya sasa na ya baadae uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano iliyokuwa chini ya Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17,2021.


Uthubutu na ujasiri wa Hayati Magufuli ulimuweka kwenye historia ya kutekeleza ndoto ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Harakati za ujenzi wa bwawa hilo zinatajwa kuanza tangu mwaka 1970 hadi 1980, ambapo Serikali ya Mwalimu Nyerere ilijaribu kutekeleza mradi huu bila mafanikio.

Kutokana na umuhimu wa mradi huo, jarida hili linachambua kwa kina hatua mbalimbali za mradi huo ambao tayari umepewa nguvu kubwa na Rais wa serikali ya Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan.


### ENEO LA MRADI

Eneo la mradi liko Kusini Mashariki mwa Pori la Akiba la Selous, pori lenye ukubwa wa zaidi ya kilometa za mraba 50,000. Mradi huo unapakana na mikoa ya Pwani na Morogoro.









VYANZO VYA MAJI VYA MTO RUFIJI AMBAVYO NDIO CHANZO KIKUU CHA MRADI WA UMEME WA MAJI RUFIJI (RHPP/JNHPP) NI MTO KILOMBERO AMBAO UNACHANGIA MAJI KIASI CHA ASILIMIA 65




### UKUBWA WA ENEO

Eneo linalotumika kwa ajili ya mradi huo limechukua kilometa za mraba 914

huku kati ya hizo eneo la shughuli za ofisi, vituo vya kupozea na kusafirisha umeme likiwa ni kilometa za mraba 61.13 na zilizobaki sehemu kubwa ni bwawa la maji.

Mgawanyo wa eneo dogo la Selous linalotumika kwa shughuli zote za mradi ni kama ifuatavyo:

Asilimia 1.8 ya pori zima la Selous ndilo lilisafishwa kwa ajili ya shughuli za mradi kwa mgawanyo huu:-

Eneo la shughuli za TANESCO kwa ajili ya ofisi na maeneo mengine ya oparesheni limechukua asilimia 0.122 na eneo lililojengwa ukuta na kutenegeneza bwawa kubwa la maji ni asilimia 1.7 tu.

Kwa upande wa eneo la kilometa nane lenye maporomoko, kipande cha maporomoko kitakachotumika kwa ajili ya mradi ni kilometa 1.3 pekee.

### VYANZO VYA MTO RUFIJI

Vyanzo vya maji vya Mto Rufiji ambavyo ndio chanzo kikuu cha Mradi wa Umeme wa JNHPP ni mto Kilombero ambao unachangia maji kiasi cha asilimia 65.

Mto Ruaha Mkuu unachangia asilimia 15 na mto Luwegu unachangia asilimia 19 ya maji yote.

Asilimia moja iliyobaki inachangiwa na vyanzo vingine vidogo vidogo.

### KUFIKA ENEO LA MRADI

Mradi unaweza kufikika kirahisi kupitia barabara, reli na usafiri wa anga. Kwa njia ya barabara kwa kutokea Dar es Salaam unaweza kupitia eneo la Ubena Zomozi ambapo ni umbali wa kilometa 340. Aidha, eneo linaweza kufikika kupitia Rufiji na Kisarawe mkoani Pwani.

### LENGO LA MRADI

Kila jambo linalofanywa na mtu, taasisi au serikali linakuwa na malengo madogo na makubwa, kwenye mradi huu wa Bwawa




la kufua umeme, lengo kuu la mradi huo ni kutekeleza azma ya kuzalisha umeme wa kutosha utakaosaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, lengo la msingi ni kuzalisha umeme wa megawati 2,115 ambao utaingizwa kwenye gridi ya taifa ili kumhakikishia mtanzania upatikanaji wa umeme wa uhakika.





# Bwawa la Nyerere mtaji kwa Taifa

### MALENGO 6 MAHUSUSI

Ukiachilia mbali mradi kuwa na lengo kuu, lakini pia yapo malengo mahususi, ambayo yanachagiza kwa kiwango kikubwa umuhimu wa mradi huo.

Malengo hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Kukamilisha mradi wa kuzalisha umeme na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa Megawati 2,115.
2. Kuanzisha miradi ya kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo la chini la mradi.
3. Kudhibiti mafuriko kwenye eneo la chini la Mto Rufiji.
4. Kuongeza usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani.
5. Kuanzisha utalii wa kupiga picha, uvuvi, na safari za boti kwenye eneo la bwawa.
6. Kuongeza udhibiti na uhifadhi wa wanyama dhidi ya ujangili.

### SERA ZA MAENDELEO ZA TAIFA

Utekelezaji wa mradi umetokana na Sera ya Nishati ya Mwaka 2015.

Sera hiyo ina lengo la kuhakikisha asilimia 75 ya Watanzania wanapata umeme wa uhakika ifikapo mwaka 2025.

Hata hivyo, kwa kuzingatia kasi na dhamira ya Serikali, lengo la awali la kisera limeongezewa nguvu zaidi kwa kuwekewa ukomo mpya, kwamba sasa wananchi wote wawe wameunganishwa na huduma ya umeme hadi kufikia mwaka 2025.

Mradi huo ni ufunguo wa kufikia malengo hayo. Aidha, Mpango Kabambe wa Sekta ya umeme umetoa maelekezo ya kimkakati ya kuendelea kubuniwa vyanzo zaidi vya uzalishaji umeme. Utekelezaji wa Mradi huo utasaidia kufikia mikakati hii lakini pia kuisaidia nchi kutimiza wajibu wake wa kidunia kupitia Malengo ya Mendeleo Endelevu (SDGs) hasa malengo mahsusi yafuatayo:

LENGO 1. Kuondoa umaskini
Lengo 7: Upatikanaji wa nishati rahisi na salama kwa mazingira.
LENGO 9: Kuendeleza Viwanda, Ubunifu na Miundombinu

### VIPENGELE VYA MRADI

Kutokana na upembuzi yakinifu uliofanywa mwaka 1980 na Kampuni za Nor Consult, Hufslund na Norplan za Norway, chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania na mapendekezo ya michoro mipya ya mwaka 2017, Mradi wa Umeme JNHPP unakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2115. Mradi huo umepita kwenye hatua mbalimbali za ujenzi wake kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa Barabara, Ofisi na huduma nyingine za kijamii.
2. Ujenzi wa Mkondo wa Mto wa muda wa chini ya ardhi kupisha ujenzi wa Bwawa Kuu.
3. Ujenzi wa Bwawa Kuu na mabwawa madogo ya kuhifadhia maji.
4. Ujenzi wa njia za kutoa maji kudhibiti ujazo wa Bwawa Kuu.
5. Ujenzi wa Kituo chenye mitambo tisa ya kuzalisha umeme;

**MANUFAA**

MANUFAA MAKUU YA MRADI HUU UTAKAPOKAMILIKA NI KUPATIKANA KWA KITUO NA CHANZO KIPYA CHA KUZALISHA UMEME KWA KUTUMIA NGUVU ZA MAJI ZA MEGAWATI 2,115 AMBAO UTAONGEZA CHACHU KWENYE UKUAJI WA UCHUMI NA MAENDELEO YA KIJAMII.







***KAMATI YA URITHI WA DUNIA YA UNESCO ILIOOMBA SERIKALI YA TANZANIA IFANYE TATHIMINI ZAIDI ITAKAYOANGALIA KWA UPANA ATHARI KWA KUFANYA TATHMINI YA KINA YA MAZINGIRA.***

**MANUFAA**

Manufaa makuu ya mradi huu utakapokamilika ni kupatikana kwa kituo na chanzo kipya cha kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji za megawati 2,115 ambao utaongeza chachu kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii. Manufaa mengine ni;-

- Kuzalisha ajira kwa Watanzania: Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi, inakadiriwa wananchi 12,000 wamepata ajira za moja kwa moja na zile za kupitia utoaji wa huduma mbalimbali. Aidha, baada ya mradi kukamilika, inatarajiwa pia kupatikana ajira za kudumu kwenye kituo kipya cha uzalishaji wa umeme;
- Bwawa Kuu linaongeza wigo wa vivutio vya utalii kama vile kuanzishwa safari za boti, utalii wa uvuvi na upigaji picha majini.
- Kubadilisha maisha ya wakazi wanaoishi ndani na nje ya eneo la mradi kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama vile kilimo, uvuvi na kilimo cha umwagiliaji. Kwa miaka mingi wakazi wa Rufiji Chini wamekuwa wakiharibiwa mazao yao kwa mafuriko wakati wa mvua au kukosa maji ya kutosha wakati wa kiangazi. Uwepo wa Bwawa Kuu unaleta ukakika wa maji ya kutosha na kuwa kinga dhidi ya mafuriko na uhakika wa kupata maji mengi zaidi yatakayotiririka baada ya kutoka kwenye mashine 9 za kuzalisha umeme ili waendeleze shughuli za kilimo cha umwagiliaji.
- Uwepo wa mradi huo na uwepo wa ofisi za mradi kutaongeza ulinzi, uhifadhi wa wanyama na kuzuia shughuli za ujangili kwenye eneo la Selous. Shughuli za awali zilizokwisha fanyika zilisaidia kuongeza idadi ya tembo katika Pori la Selous.
- Faida ya moja kwa moja kwa Serikali ni kupata mapato yatokanayo na ushuru wa forodha na uuzaji wa umeme kwa wakandarasi wakati wa utekelezaji wa mradi.



**Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi, inakadiriwa wananchi 12,000 wamepata ajira za moja kwa moja na zile za kupitia utoaji wa huduma mbalimbali**











SERIKALI YA TANZANIA KWA KUTAMBUA UMUHIMU WA MAZINGIRA ILITOA KAZI KWA WATAALAMU HURU KUFANYA UPEMBUZI YAKINIFU WA ATHARI ZA KIJAMII NA KIMAZINGIRA (ESIA). MATOKEO YA TATHMINI HIYO YALITOLEWA MEI, 2018 NA KUBORESHWA ZAIDI OKTOBA, 2018

### VIKWAZO

Awali mradi huu ulikumbana na vikwazo kadhaa kutoka kwa watetezi wa masuala ya mazingira na uhifadhi hasa UNESCO na WWF.

Watetezi hao walikuwa na hofu kuwa huenda maisha ya mimea na wanyama kwenye eneo la ekolojia inayozunguka Selous kama eneo la Urithi wa Dunia na maisha ya wanyama na mimea kwenye Pori la Akiba la Selous vitaathiriwa na utekelezaji wa mradi huo.

Serikali ya Tanzania kwa kutambua umuhimu wa mazingira ilitoa kazi kwa wataalamu huru kufanya upembuzi yakinifu wa athari za kijamii na kimazingira (ESIA). Matokeo ya tathmini hiyo yalitolewa Mei, 2018 na kuboreshwa zaidi Oktoba, 2018, yalionesha kuwa mradi huu ni muhimu kwa maisha na uchumi wa Tanzania na kwamba athari chache za kimazingira zinadhibitika kwa kuweka mpango mahsusi wa kurekebisha athari hizo.

Kamati ya Urithi wa Dunia ya UNESCO ilioomba Serikali ya Tanzania ifanye tathmini zaidi itakayoangalia kwa upana athari kwa kufanya tathmini ya kina ya Mazingira. Serikali iliweka wazi kuwa michoro ya Bwawa Kuu la uzalishaji wa umeme ilifahamika kwa UNESCO hata kabla ya eneo la Selous kupewa hadhi ya Urithi wa Dunia. Michoro ilikamilika mwaka 1980,na Pori la Akiba la Selous liliwekwa kwenye orodha ya UNESCO mwaka 1982.

Ukweli ni kwamba mradi huu utaleta faida kubwa kwa Taifa.

Mradi huu utachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za bei ya umeme nchini kwani uzalishaji wake ni wa gharamanafuu tofauti na vyanzo vingine kama vinavyoonekana hapo chini.



GHARAMA ZA UZALISHAJI UMEME KWA NJIA MBALIMBALI KWA

## uniti MOJA




**Wakuu wa Mashirika msiogope kufanya mabadiliko, wawekeni watu ambao watakwenda na kasi tunayoitaka**



RAIS

# SAMIA:

## JNHPP ILINIUMIZA KICHWA

MITAMBO KUANZA KUWASHWA 2024 ILI KUZALISHA UMEME WA MAJARIBIO

RAIS Samia Suluhu Hassan ameweka wazi kuwa moja ya mambo yaliyomuumiza kichwa mara baada ya kukalia kiti cha urais Machi 19, 2021 ni miradi mikubwa ya kimkakati, ukiwemo wa bwawa la kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP). Aliyasema hayo Februari 14, 2023 mara baada ya kushuhudia shughuli ya utiaji saini wa mkataba wa miradi 26 ya utekelezaji wa miradi mahususi ya umeme yenye thamani ya shilingi trilioni 1.9, iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Miradi hiyo ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Gridi ya taifa na transfoma 66 zinatarajiwa kununuliwa na waya zenye urefu wa kilomita 6,502. Pamoja na mambo mengine, Rais alisema hakujua atapata wapi fedha za kuendesha mradi huo pamoja na mradi wa reli ya kisasa ya SGR.

Alisema kwa kuwa alikuwa na nia basi alifanikiwa kupata njia na hatimae leo hii mradi wa JNHPP unakwenda vizuri na kuna uwezekano mkubwa mapema mwakani mitambo ikaanza kuwashwa na kuzalisha umeme wa awali wa majaribio. “Nilipoingia madarakani, Mradi wa umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere na SGR viliniumiza kichwa, sikujua nitapata wapi fedha, leo SGR kuna fedha mpaka ya kufika Kigoma na bwawa la Nyerere nadhani mapema mwakani tutaanza kuwasha mitambo na kuzalisha umeme wa awali wa majaribio.Penye nia pana njia.”

### KUWAJALI WANYONGE

Katika hoyuba yake Rais Samia aliipongeza Wizara ya Nishati, REA na TANESCO kwa kuandaa miradi muhimu itakayoleta ustawi wa nchi yetu na watu wake na kuweka wazi kuwa huko ndio kuwajali wanyonge. “Kati ya mikataba tuliyosaini upo wa kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji wadogo wadogo, maeneo ya kilimo, viwanda vidogo, vituo vya afya na kwenye vyanzo vya maji, huku ndio kuwajali wanyonge na sio kusimama kuwaongelea na kuzidi kuwatia unyonge. Alisema miradi miwili ya TANESCO na REA inakwenda pamoja kwani bila kuimarisha Gridi ya Taifa, juhudi kubwa zinazoendelea za kusambaza umeme vijijini hazitaweza kuzaa matunda.

### USALAMA VIJIJINI

Rais alisema kupatikana kwa umeme wa uhakika kutasaidia kuimarisha usalama kwenye maeneo yote ya nchi. “Miradi hii ya umeme itakapokamilika itaimarisha usalama vijijini, wale wanaofanya uovu hawatathubutu kufa nya hivyo. “Ni dhamira ya Serikali kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Watanzania wote, mijini na vijijini kwa kuwapatia huduma bora. Huduma nyingine pia zitawafikia wananchi kwa njia ya TEHAMA. “TEHAMA inakuza maendeleo haraka, hivyo tukipeleka umeme na TEHAMA vijijini, hata wale Wakurugenzi wanaoleta taarifa za uongo hazitakuwepo maana mifumo ya kuripoti itafika mpaka vijijini.”

### UTEUZI WA WAKANDARASI

Akizungumzia uteuzi wa wakandarasi, Rais alisema umefanywa kwa umakini mkubwa, ili miradi hii ifanyike haraka na tupate maendeleo ya haraka kunahitajika maamuzi ya haraka.

NILIPOINGIA MADARAKANI, MRADI WA UMEME WA BWAWA LA MWALIMU NYERERE NA SGR VILINIUMIZA KICHWA, SIKUJUA NITAPATA WAPI FEDHA, LEO SGR KUNA FEDHA MPAKA YA KUFIKA KIGOMA NA BWAWA LA NYERERE NADHANI MAPEMA MWAKANI TUTAANZA KUWASHA MITAMBO NA KUZALISHA UMEME WA AWALI WA MAJARIBIO.PENYE NIA PANA NJIA



**Uunganishwaji na usambazaji wa umeme vijijini unategemea vyanzo vizuri vya uzalishaji na kazi hiyo inafanywa kwa nguvu kubwa na serikali**

**2025 TUTAFIKISHA MW 5,000**

MWAKA WA FEDHA 2022/23, SERIKALI IMETENGA SHILINGI BILIONI 500 KWA AJILI YA KUANZA AWAMU YA KWANZA AMBAYO NI KATI YA SHILINGI TRILIONI 1.9 INAYOTAKIWA KWA AWAMU YOTE YA KWANZA ILI KUTEKELEZA MIRADI 26 YA KUIMARISHA GRIDI NCHINI."

"Wakandarasi mnaokosa tenda mkianza kuzunguka PCCCB ama PPRA mnazuia miradi na utendaji kwenda haraka."

#### URASIMU KWENYE AJIRA

Kwenye eneo hili Rais Samia alisema kuna mashirika ambayo yanahitaji ajira za haraka lakini mlolongo wa kupata watu unakuwa mrefu na kwamba kama taasisi zinataka wafanyakazi, mishahara ya kulipa wanayo haitoki hazina ni vema wakapewa ruhusa ya kuajiri ili miradi ikatekelezwe kwa haraka.

"Wakuu wa Mashirika msiogope kufanya mabadiliko, wawekeni watu ambao watakwenda na kasi tunayoitaka."

#### VYANZO VIZURI VYA UZALISHAJI

Alisema uunganishwaji na usambazaji wa umeme vijijini unategemea vyanzo vizuri vya uzalishaji na kazi hiyo inafanywa kwa nguvu kubwa na serikali.

#### MAKAMBA: TATIZO LA UMEME KUWA HISTORIA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amebainisha kuwa kutokana na kasi ya miradi ya kuzalisha umeme nchini ukiwemo wa Bwala la Mwalimu Nyerere (JNHPP) ana uhakika hadi kufikia mwaka 2025 changamoto ya umeme itakuwa imekwisha kabisa.

"Tunakuhakikishia Rais Dkt. Samia kuwa ifikapo mwaka 2025 tutafikisha MW 5,000 ambazo ni mara tatu ya umeme uliopo leo, hatua hii itamaliza tatizo la umeme nchini".

Alisema katika kutekeleza mradi wa Gridi imara, hii ni awamu ya kwanza, hivyo wale ambao wana changamoto za umeme katika maeneo yao na hayajatajwa wasinyong'onyee kwani ziko awamu za mradi huu zinazoendelea, mradi huu unagusa nchi nzima.

"Tuna miradi mikubwa ya usafirishaji na uzalishaji ambayo tunaendelea nayo, miradi ya uzalishaji ukiwemo wa Bwawa la Julius Nyerere na miradi ya kuzalisha umeme wa upepo na jua ambapo tutaanza na mkoa wa Shinyanga eneo la Kishapu MW 150 za umeme wa jua tutaziingiza kwenye Gridi ya Taifa mwakani.

"Miradi ya uzalishaji umeme kwa kutumia nguvu ya maji ambayo tayari imeshapata fedha ikiwemo wa Kakoro (Kagera), Malagarasi (Kigoma) na Rusumo. Aidha, kuna miradi ya gesi ambayo itatupatia MW 600 za umeme ifikapo mwisho wa mwaka ujao."

MRADI WA TATU NI WA KUPELEKA UMEME KWENYE VITUO VYA AFYA NA PAMPU ZA MAJI KWA MAENEO YA VIJIJINI KATIKA MIKOA YOTE TANZANIA

Makamba alisema hatua hiyo ni uamuzi wa kijasiri na kishupavu wa Rais Samia kwa lengo la kuhakikisha shida za umeme zinaisha.

**KAULI YA MAHARAGE CHANDE**

KWA upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, alisema ongezeko la mahitaji ya umeme ni asilimia 11 mwaka hadi mwaka na kwamba kwa upande wao ongezeko hilo limekumbana na changamoto nyingi.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo kumekuwa na miradi mbalimbali ya kujaribu kuongeza ubora na uhakika wa umeme.

"Miongoni mwa miradi hiyo ni wa kuimarisha Gridi ya Taifa, na mwaka jana tulifanya tathmini na kupata kibali cha kuanzisha mradi huo na kuuita Gridi Imara.

"Tathmini ya awali ilionesha kuwa mradi wa Gridi Imara unahitaji Shilingi trilioni 4.42 ili kuhakikisha gridi inakuwa ya uhakika.

"Mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetenga Shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kuanza awamu ya kwanza ambayo ni kati ya Shilingi trilioni 1.9 inayotakiwa kwa awamu yote ya kwanza ili kutekeleza miradi 26 ya kuimarisha gridi nchini."

Alisema mradi wote wa Gridi Imara utatekelezwa kwa miaka minne ambapo awamu ya kwanza itatekelezwa kwa miaka miwili.

Aliongeza kuwa tangu REA ianzishwe, imekuwa ikifadhili na kusimamia miradi mbalimbali ambapo iliweza kupandisha hali ya upatikanaji wa umeme vijijini kutoka asilimia 5 mwaka 2007 mpaka asilimia 69 hivi sasa.

"Kati ya vijiji 12,345, vijiji 9,467 vimeshafikiwa na huduma za umeme, vijiji 2,878 vilivyobaki Wakandarasi wapo wanaendelea na kazi.

"Kati ya vitongoji 64,760 vya Tanzania, vitongoji 28,424 vimeshafikiwa na huduma za umeme na vitongoji 36, 336 vilivyobakia vinafanyiwa kazi."

**VYANZO VYA FEDHA**

Chande alisema Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya na Ufaransa wameweza kutenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 385 ili kutekeleza miradi mitatu mikubwa.

Mradi wa kwanza ni wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 1,522 (mradi wa ujazilizi) ambao una thamani ya bilioni 234 ambazo ni fedha za Serikali kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Ufaransa. "Mradi huu unategemewa kuunganisha umeme kwa wananchi 88,200."

Mradi wa pili ni wa kupeleka umeme kwenye migodi na maeneo yenye shughuli za kilimo ambao utagharimu Shilingi bilioni 115 fedha za Serikali kwa 100%, utapeleka huduma kwenye maeneo 336 katika mikoa yote Tanzania Bara lengo lake likiwa ni kupunguza gharama za uchimbaji hasa wachimbaji wadogo.

Mradi wa tatu ni wa kupeleka umeme kwenye vituo vya afya na pampu za maji kwa maeneo ya vijijini katika mikoa yote Tanzania Bara, utafikisha umeme kwenye vituo vya afya 63 na pampu za maji 333. "Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Jumuiya ya Ulaya ambayo ilitupatia Dola za Marekani milioni 15.

"Ndani ya mwaka huu wa fedha tunatarajia kusaini mikataba ya miradi mingine mitatu mikubwa ambayo itapeleka umeme vijijini ukiwemo mradi wa kupeleka umeme pembezoni mwa miji katika mitaa 416 katika mikoa nane ambao utagharimu Shilingi bilioni 76.9.

"Tunakushukuru Rais wetu na Serikali yetu, tangu umeingia madarakani, Wakala umeweza kusaini miradi ya Shilingi trilioni 2.2 ambapo kati ya fedha hizo,

TUNAKUHAKIKISHIA RAIS DKT. SAMIA KUWA IFIKAPO MWAKA 2025 TUTAFIKISHA MW

# 5,000



WAZIRI WA NISHATI, JANUARY MAKAMBA









LENGO

LENGO LA KUANZISHA MRADI HUU NI MOJA YA JUHUDI ZA SERIKALI ZA KUPUNGUZA GHARAMA ZA UMEME KWA WANANCHI KWA SABABU UZALISHAJI WAKE NI WA GHARAMA NAFUU UKILINGANISHA NA VYANZO VINGINE.

MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP MPANGO







# FEDHA
## ZA MRADI WA JNHPP ZIPO

Dhamira ya serikali ni kuhakikisha mradi huo unakamilika kama ilivyopangwa.

DHAMIRA YA SERIKALI AWAMU YA 6



MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDOR MPANGO



KUKAMILIKA KWA MRADI HUO KUTAWAWEZESHA WATANZANIA KUPATA UMEME MWINGI NA WA GHARAMA NAFUU AMBAO UTASAMBAZWA NCHINI KOTE NA ZIADA KUUZWA NJE YA NCHI ILI KULIPATIA TAIFA FEDHA ZA KIGENI.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kutoa fedha za kugharamia ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), ili ukamilike kwa wakati.

Hiyo imekuwa ni ahadi ya Rais Samia mwenyewe, lakini pia wasaidizi wake wamekuwa mstari wa mbele kuisimamia ahadi hiyo.

Miongoni mwao ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango, ambaye alitueleza umma kuwa fedha za kukamilisha mradi huo na miradi mingine yote zipo.

Dkt. Mpango pia alipongeza wizara ya Nishati, Wakandarasi pamoja na wafanyakazi wote wanaoshiriki katika ujenzi wa mradi huo. Alisema mradi huo ni mkombozi katika sekta ya nishati nchini hivyo amewataka viongozi na wote wanaohusika katika mradi huo kuwa wazalendo na kutanguliza maslahi ya taifa wakati wote.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha mradi huo unakamilika kama ilivyopangwa na kuwaagiza wakandarasi kuwa makini na kutatua hitilafu yeyote itakayojitokeza mapema ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza baadae katika mradi huo.

Aidha aliwaagiza viongozi wa mikoa na wilaya zote inakopita mito inayotiririsha maji katika mto Rufiji kutunza mito hiyo na kutoa elimu kwa wananchi ili kulinda mazingira kwa manufaa ya mradi huo.

Kukamilika kwa mradi huo kutawawezesha Watanzania kupata umeme mwingi na wa gharama nafuu ambao utasambazwa nchini kote na ziada kuuzwa nje ya nchi ili kulipatia Taifa fedha za kigeni.

Bwawa hilo linatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 ambazo zikijumlishwa na megawati 1,500 zinazozalishwa na vyanzo mbalimbali nchini hivi sasa zitaifanya Tanzania kuwa na umeme utakaotosheleza mahitaji yake na ziada kuuzwa kwa majirani.

**MRADI HUU NI MKOMBOZI KATIKA SEKTA YA nishati NCHINI**





# MABADILIKO

## Tabia nchi

**Sote tunapaswa kuwajibika kutunza mazingira kwa minajili ya vizazi vya leo na vya kesho**

TZ&BEYOND

AIDHA WANANCHI WANAOZUNGUKA MRADI HUO WANAPASWA KUENDELEA KUTOA USHIRIKIANO KWA WAJENZI KWA KUWAHAKIKISHIA USALAMA WAO, MALI ZAO NA VIFAA VINAVYOTUMIKA KATIKA UJENZI HUO.


"Lengo la kuanzisha mradi huu ni moja ya juhudi za Serikali za kupunguza gharama za umeme kwa wananchi kwa sababu uzalishaji wake ni wa gharama nafuu ukilinganisha na vyanzo vingine.

Uniti moja ya umeme unaozalishwa kwa kutumia maji inagharimu shilingi 36 hadi shilingi 50 huku umeme unaotumia vyanzo vya mafuta uniti moja inazalishwa kwa gharama ya shilingi 440 hadi shilingi 600."

Faida nyingine ya ujenzi wa mradi huo ni pamoja na kuzalisha ajira kwa Watanzania mbalimbali wanaoshiriki katika kuujenga na kutoa huduma mbalimbali kama wauzaji wa vifaa vya ujenzi, mafuta, vyakula na huduma nyingine zinazohitajika kwenye mradi huo.

Imeelezwa kuwa tayari kazi ya ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka kwenye chanzo cha mradi huo hadi Chalinze mkoani Pwani na ukifika Chalinze njia moja itakwenda Dar es Salaam na nyingine Dodoma ili kuwezesha umeme huo kusambazwa nchi nzima inaendelea.

Aidha wananchi wanaozunguka mradi huo kuendelea kutoa ushirikiano kwa wajenzi kwa kuwahakikishia usalama wao, mali zao na vifaa vinavyotumika katika ujenzi huo.














**FAIDA**

FAIDA YA UJENZI WA MRADI HUO NI PAMOJA NA KUZALISHA AJIRA KWA WATANZANIA MBALIMBALI WANAOSHIRIKI KATIKA KUUJENGA NA KUTOA HUDUMA MBALIMBALI KAMA WAUZAJI WA VIFAA VYA UJENZI, MAFUTA, VYAKULA NA HUDUMA NYINGINE ZINAZOHITAJIKA KWENYE MRADI HUU.





UMEME VIJIJINI

KATI YA VITONGOJI 64,760 VYA TANZANIA, VITONGOJI 28,424 VIMESHAFIKIWA NA HUDUMA ZA UMEME NA VITONGOJI 36, 336 VILIVYOBAKIA VINAFANYIWA KAZI.





## MRADI WA PILI

Mradi wa pili ni wa kupeleka umeme kwenye migodi na maeneo yenye shughuli za kilimo ambao utagharimu Shilingi bilioni 115 fedha za Serikali kwa 100%, utapeleka huduma kwenye maeneo 336 katika mikoa yote Tanzania Bara lengo lake likiwa ni kupunguza gharama za uchimbaji hasa wachimbaji wadogo.




**Ndani ya mwaka huu wa fedha tunatarajia kusaini mikataba ya miradi mingine mitatu mikubwa ambayo itapeleka umeme vijijini ukiwemo mradi wa kupeleka umeme pembezoni mwa miji katika mitaa 416 katika mikoa nane ambao utagharimu Shilingi bilioni**

# 76.9



**RAIS SAMIA**

AJAZA MAJI BWAWA LA JNHPP

# HISTORIA IMEANDIKWA

**Kama tulivyojuzwa hapo awali, hadi sasa kazi imekamilika kwa asilimia 78.68%, kinachoendelea hivi sasa ni kufunga mitambo ya kufua umeme na vifaa vingine kabla hatujaenda kwenye majaribio ya kuiwasha.**




MAENDELEO

MRADI HUU UTATULETEA UMEME WA UHAKIKA KWA AJILI YA MAENDELEO ENDELEVU NA KUTIMIZA NDOTO ILIYOKUWEPO TANGU TUMEPATA UHURU, TUNAWASHUKURU WOTE WALIOSHIRIKI KULETA FIKRA HII NA WALIOSHIRIKI KATIKA UTEKELEZAJI WAKE.

NA JIMMY KIANGO

MWISHONI mwa mwaka 2022 nchi iliandika historia ambayo haitakuja kufutika kamwe. Rais Samia Suluhu Hassan alishiriki katika kukamilisha ndoto ya muda mrefu ya kuwa na nishati ya umeme wa uhakika kwa kushiriki kikamilifu zoezi la kufunga lango la njia ya mchupusho wa maji ili kuruhusu ujazaji wa maji katika bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP). Hatua ya kulijaza bwawa hilo inatarajiwa kuchukua misimu miwili ya mvua, ambapo bwawa hilo linatarajiwa kukamilika na kuanza kazi ya awali mwaka 2024. Hadi kufikia Desemba 22, 2022 ujenzi wa bwawa hilo lenye ukubwa wa meta za ujazo 32.3 ulikuwa umekamilika kwa asilimia 78.68.

Akizundua hatua hiyo ya kujaza maji kwenye bwawa hilo ambalo ujenzi wake uliasisiwa na Hayati Rais Dkt. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 2021, Rais Samia alisema hili ni tukio muhimu la kihistoria na faraja nchini kwetu katika safari ya kukamilisha mradi wa bwawa hilo. Alisema hatua hiyo inatoa ujumbe duniani kuwa Tanzania inaweza kutekeleza mambo makubwa ya kuweza kubadilisha taswira ya nchi na ulimwengu pamoja na kuweka alama mpya katika ramani ya dunia.



"WAKATI NAPEWA JUKUMU LA KUONGOZA NCHI HII MRADI HUU ULIKUWA ASILIMIA 37%, NA LEO NAMSHUKURU MUNGU KUONA UMEFIKIA 78.68%,

**Ujenzi wa Bwawa la Nyerere ni kazi kubwa yenye ubora na viwango vinavyotakiwa**

"Mradi huu utatuletea umeme wa uhakika kwa ajili ya maendeleo endelevu na kutimiza ndoto iliyokuwepo tangu tumepata Uhuru, tunawashukuru wote walioshiriki kuleta fikra hii na walioshiriki katika utekelezaji wake.

"Nawapongeza sana Wizara ya Nishati, TANESCO, Katibu Mkuu Kiongozi, kampuni, benki, TANAPA, TAWA, TFS, TANROADS, vyombo vya Ulinzi na Usalama, wadau wote wa maendeleo pamoja na wote wanaosaidiana nao kwa kazi nzuri ya usimamizi na utekelezaji inayoendelea kufanywa.

"Ujenzi wa Bwawa la Nyerere ni kazi kubwa yenye ubora na viwango vinavyotakiwa, safari ya ujenzi ilianza kipindi cha Hayati Mwalimu Nyerere na katika kipindi cha Awamu ya Tano cha Hayati John Pombe Magufuli ujenzi ulianza kutekelezwa, pamoja na mikiki mikiki iliyokuwepo kuhusu suala hili, lakini kazi ilianza na kupelekea matunda tunayoyaona hivi leo.

"Naishukuru sana Serikali ya Misri kwa kuwa pamoja nasi, salaam zimfikie Rais wa Misri, Mhe. Abdel Fattah El-Sisi kwa ushirikiano mkubwa anaotupa kwa kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo.

"Wakati napewa jukumu la kuongoza nchi hii mradi huu ulikuwa asilimia 37%, na leo namshukuru Mungu kuona umefikia 78.68%, natoa ahadi kwenu ndugu Watanzania kuwa nitausimamia mradi huu hadi ukamilike kama ulivyopangwa.

"Kama tulivyojuzwa hapo awali, hadi sasa kazi imekamilika kwa asilimia 78.68%, kinachoendelea hivi sasa ni kufunga mitambo ya kufua umeme na vifaa vingine kabla hatujaenda kwenye majaribio ya kuiwasha.

Aliongeza kuwa mradi huo ni mojawapo ya miradi mikubwa barani Afrika na kwamba Watanzania wanayo kila sababu ya kujivunia uwekezaji huu wenye faida nyingi zikiwemo za kuweka akiba kubwa ya maji na kuzalisha umeme hata kama mvua imepungua na kusaidia kudhibiti mafuriko ya mara kwa mara ya mto Rufiji.









MANUFAA YA BWAWA HILI KATIKA NYANJA ZOTE YATAWEZEKANA KAMA TUTATUNZA MAZINGIRA KATIKA VYANZO NA MABONDE YA MITO INAYOLETA MAJI HAPA BWAWANI, TUTUNZE MAZINGIRA MAANA HUU MRADI TUMEUJENGA KWA GHARAMA KUBWA

Alisema mradi pia utasaidia katika kilimo cha uhakika cha umwagiliaji, utaimarisha na kufungua fursa nyingi za utalii katika eneo la Kusini mwa Tanzania hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na hivyo kutoa ajira za moja kwa moja na nyinginezo.

"Kupitia Bwawa hili, tumejenga daraja kubwa na bora kuiunganisha mikoa ya Kusini, kilichobakia ni barabara ambapo nawaelekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (TANROADS) kuandaa mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Chalinze hadi Utete kupitia kwenye daraja hili, lengo ni watu wanaotoka Mtwara na Lindi kwenda Dodoma, Iringa au Arusha hatakuwa na haja ya kupitia Dar es Salaam hivyo njia hii itafupisha sana safari hizo.

**MAELEKEZO**

Katika zoezi hilo lililofanyika Rufiji, mkoani Pwani, Rais alitoa maelekezo kwa wizara kadhaa.

"Naielekeza Wizara ya Uvuvi na Mifugo kuja na mipango mkakati ya ufugaji wa kisasa wa samaki ili tukuze uchumi wa watu wetu wa maeneo haya.

Naielekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, TAMISEMI na mamlaka nyinginezo mkapime maeneo hayo kwa kuyaweka kwenye mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya mnada wa uwazi kwa wawekezaji wa uhakika katika kilimo, pia kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo yatakayokuwa na miundombinu ya umwagiliaji.

"Manufaa ya bwawa hili katika nyanja zote yatawezekana kama tutatunza mazingira katika vyanzo na mabonde ya mito inayoleta maji hapa bwawani, tutunze mazingira maana huu mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kujinyima vitu vingi muhimu, hivyo tuutunze kufa au kupona.

**UKUBWA WA MRADI**

MRADI HUU NI MOJAWAPO YA MIRADI MIKUBWA BARANI *Afrika*



Mkuu wa Mkoa Pwani ABUBAKAR KUNENGE

Waziri wa Nishati JANUARY MAKAMBA

Spika wa Bunge Dkt. TULIA ACKSON

Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar SHAIBU HASSAN KADUARA

Mkurugenzi Mtendaji Tanesco MAHARAGE CHANDE

# KUTOKA KWA VIONGOZI MBALI MBALI

HISTORIA

## RAIS SAMIA AJAZA MAJI BWAWA LA JNHPP

UTEKELEZAJI WA MRADI HUU HAUGUSI TU KWENYE ENEO LA KULETA SULUHU YA KUDUMU KWA UPATIKANAJI WA UHAKIKA WA UMEME LAKINI PIA UNAGUSA KWENYE SEKTA NYINGINE MUHIMU YA UPATIKANAJI WA UHAKIKA WA MAJI KWA MIKOA ILIYOPO KARIBU NA BWAWA HILI.

### SPIKA DKT. TULIA ACKSON: TUMEPATA SULUHU YA KUDUMU

Akishiriki zoezi hilo, Spika wa Bunge, Dkt Tulia Ackson, alisema nchi imetengeneza historia ya kuondoa tatizo la umeme na kwamba hatua hiyo ni suluhu ya kudumu.

"Niseme tu Rais Samia umefanya, unafanya na kuzidi, hivyo nakupongeza sana. "Utekelezaji wa mradi huu haugusi tu kwenye eneo la kuleta suluhu ya kudumu kwa upatikanaji wa uhakika wa umeme lakini pia unagusa kwenye sekta nyingine muhimu ya upatikanaji wa uhakika wa maji kwa mikoa iliyopo karibu na bwawa hili.

"Kwa wingi wa maji haya, tunaamini tutakuwa na uhakika wa kupata chakula cha kutosha cha kulisha Taifa letu na dunia nzima kwani maji yatawasaidia wakulima kumwagilia mazao yao kwa uhakika."

### JANUARY MAKAMBA ATOA SHUKURANI

Waziri wa Nishati, January Makamba alitoa shukurani kwa Rais Samia kwa uongozi wake madhubuti na ushahidi ni kuonekana kwa matokeo ya ustawi wa Watanzania pamoja na kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu, umoja, upendo na mapatano. "Kwa mujibu wa mkataba, pale fedha zinapochelewa kulipwa kwa kila hatua huwa kuna adhabu, hatujawahi kuchelewa hata mara moja kufanya malipo ya mradi huu na hadi leo hii hatudaiwi fedha yoyote.

"Rais Samia ulipoingia madarakani mradi huu ulikuwa umefikia 37%, katika kipindi cha miezi 20 ya uongozi wako, mradi huu umefikia 78%, tunakushukuru kwa kuusukuma kwa kasi mradi huu.

### KAULI YA WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI - ZANZIBAR, SHAIBU HASSAN KADUARA

"Na sisi ni sehemu ya watu tutakaonufaika na uzalishaji wa umeme huu, hivi karibuni tuliondoa changamoto ya muungano ambapo tumekubaliana kuuziana umeme kwa bei nafuu ya Shilingi 130 kwa Uniti moja.

"Tunaendelea kukushukuru na kukupongeza kwa kusimamia kwa dhati muungano wetu, tunawapongeza pia TANESCO kwa ushirikiano mkubwa na Shirika letu la Umeme la ZECO.



**MAHARAGE CHANDE**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO**

NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI INA UREFU WA MITA 703 NA UPANA WA KIPENYO CHA MITA 12, KWA UPANDE WA UJENZI WA TUTA KUU UMEFIKIA 89.51% HUKU 10.5% ZILIZOBAKI NI KUMALIZIA MAGETI ILI BWAWA LINAPOJAA MAGETI YAFUNGULIWE MAJI YAWEZE KUTOKA.

UKUTA UNA UWEZO WA KUHIFADHI MAJI LITA

**BILIONI 32**

### MAHARAGE CHANDE ATOA NENO

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la umeme nchini (Tanesco) Maharage chande alisema njia ya kwanza ya mradi huu ilikuwa ni njia ya kuchepusha maji ya mto na ujenzi wa njia ya mchepusho wa maji umefikia 97.97% na 3.2% iliyobaki kumalizika ni kazi ya kufunga lango kuu ya njia ya mchepusho wa maji ambayo imeshafanyika.

"Njia ya kuchepusha maji ina urefu wa mita 703 na upana wa kipenyo cha mita 12, kwa upande wa ujenzi wa tuta kuu umefikia 89.51% huku 10.5% zilizobaki ni kumalizia mageti ili bwawa linapojaa mageti yafunguliwe maji yaweze kutoka. "Ukuta una uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 32, maji haya ni mengi zaidi ya maji yanayopatika ziwa Rukwa yakishajaa katika tuta. Huku maji yanayopita katika njia moja ya mashine ni takriban lita 225,000 kwa sekunde.

"Usimikaji na ufungaji mitambo kwenye jengo la kufulia umeme umefikia 60.46%, ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirisha umeme umefikia 97.20%.

"Ujenzi wa njia ya kupitisha umeme umefikia 80%, ujenzi wa daraja litakalounganisha mikoa ya kusini na kaskazini umefikia 96.87% na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi umefikia 84.89%.

"Mradi huu unakadiriwa kutumia Shilingi trilioni 6.5 ambazo ni fedha zetu zinazotokana na kodi za Watanzania ambapo mpaka kufikia Novemba 2022, Serikali imemlipa Mkandarasi Shilingi trilioni 4.5 sawa na 70% za mradi.

"Hadi kufikia mwezi Novemba, 2022, mradi huu umeajiri watu 12,275 ambapo kati ya walioajiriwa, Watanzania ni 11,164 sawa na 90.97%.

"Mradi huu umejengwa kwa kuzingatia mazingira kama miradi mingine ili usilete athari za mazingira. Ukuta uliojengwa kwenye mradi huu una matundu ambayo yatapitisha maji kidogo ili kuhakikisha viumbe na maisha nyuma ya ukuta yanaendelea.

### ABUBAKAR KUNENGE

"Nishati ni muhimu sana kwa mkoa huu kwani ni mkoa wa uwekezaji na biashara, mkoa wa viwanda na kilimo, yote haya yanahitaji zaidi nishati ya umeme, maji na barabara n.k

"Bwawa hili lina fursa nyingi, sisi wakazi wa Pwani tumejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama wa eneo hili unakuwa ni kipaumbele chetu pia tutalinda mazingira pamoja na vyanzo vya maji.

### FATMA MWASSA

"Nawakaribisha wote mliojumuika hapa katika kuweka historia ya nchi yetu. Kipekee, tunakushukuru na kukupongeza Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza kutekeleza kwa kasi kubwa mradi huu mkubwa wa bwawa la Julius Nyerere mpaka kufikia hatua hii ambapo utafunga njia ya mchepusho wa maji ya bwawa hili.

"Mradi wa bwawa la Mwalimu Nyerere utakapokamilika, 93% ya umeme unaozalishwa nchini kote utakuwa unazalishwa Morogoro kupitia mabwawa ya Kihansi, Kidatu na JK Nyerere.

MRADI HUU UMEJENGWA KWA KUZINGATIA MAZINGIRA KAMA MIRADI MINGINE ILI USILETE ATHARI ZA MAZINGIRA

UKUTA ULIOJENGWA KWENYE MRADI HUU UNA MATUNDU AMBAYO YATAPITISHA MAJI KIDOGO ILI KUHAKIKISHA VIUMBE NA MAISHA NYUMA YA UKUTA YANAENDELEA.



JULIUS NYERERE UTABAKI KUWA NI MOJA YA MRADI MKUBWA WA KIMAENDELEO KATIKA

**bara letu**

# *MISRI*

## YAACHA UJUMBE MZITO

WAZIRI WA MAMBO YA NJE WA SERIKALI YA MISRI  SAMEH SHOUKRI, ALIACHA UJUMBE MZITO KWA TANZANIA KWA KUWEKA WAZI KUWA MRADI HUO NI MUHIMU NA UNAPASWA KULINWA NA WATANZANIA WOTE.

“NAIPONGEZA SERIKALI YA TANZANIA KWA JITIHADA KUBWA AMBAZO IMEZIFANYA KWA KUTHUBUTU KUANZISHA MRADI HUU, KWA SASA UMEFIKIA 78%, TUKIO HILI LA UJAZAJI WA MAJI NI HATUA KUBWA KATIKA KUFANIKISHA MRADI HUU.

“TANZANIA IMEWEKEZA JUMLA YA DOLA ZA MAREKANI BILIONI 2.9 KWA AJILI YA KUZALISHA UMEME WA MEGAWATI 2115, MRADI WA KUFUA UMEME WA BWAWA LA JULIUS NYERERE UTABAKI KUWA NI MOJA YA MRADI MKUBWA WA KIMAENDELEO KATIKA BARA LETU.




# Ajira
## kwa wananchi

HADI KUFIKIA MWEZI NOVEMBA, 2022, MRADI HUU UMEAJIRI WATU 12,275 AMBAPO KATI YA WALIOAJIRIWA, WATANZANIA NI 11,164 SAWA NA 90.97%. MRADI HUU UMEJENGWA KWA KUZINGATIA MAZINGIRA KAMA MIRADI MINGINE ILI USILETE ATHARI ZA MAZINGIRA. UKUTA ULIOJENGWA KWENYE MRADI HUU UNA MATUNDU AMBAYO YATAPITISHA MAJI KIDOGO ILI KUHAKIKISHA VIUMBE NA MAISHA NYUMA YA UKUTA YANAENDELEA.


# TZ&BEYOND




***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI

www.tz&beyond.co.tz



# Bwawa la NYERERE LAFIKIA 80.2%

### MRADI UNAKWENDA KWA KASI

HAYO YALIBAINISHWA NA NAIBU WAZIRI WA NISHATI, WAKILI STEPHEN BYABATO, KWA KUSEMA KUWA MRADI HUO UTAKAOZALISHA MEGAWATI 2,115 SASA UNAKWENDA KWA KASI.

BYABATO ALIYASEMA HAYO JANUARI 17, 2023 WAKATI WIZARA YA NISHATI IKITOA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI HUO KWA WAJUMBE WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI JIJINI DODOMA.





# Bwawa la NYERERE LAFIKIA 80.2%



KWA SASA UTEKELEZAJI WA MRADI UNAPENDA KASI AMBAPO HADI KUFIKIA DESEMBA 31,2022 MRADI ULIKUWA UMEFIKIA ASILIMIA 80.22 YA UJENZI




NAIBU WAZIRI WA NISHATI, WAKILI STEPHEN BYABATO



Utekelezaji wa mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere maarufu kama JNHPP umefikia asilimia 80.2. Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, kwa kusema kuwa mradi huo utakaozalisha megawati 2,115 sasa unakwenda kwa kasi. Byabato aliyasema hayo Januari 17, 2023 wakati Wizara ya Nishati ikitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

"Kwa sasa utekelezaji wa mradi unaenda kwa kasi ambapo hadi kufikia Desemba 31, 2022 umefikia asilimia 80.22,





aidha mnamo Desemba 22, 2022 zoezi la kuanza kujaza maji katika bwawa la JNHPP lilifanyika kwa kufunga mageti ya njia ya mchepusho."

Kuhusu kazi ya ujazaji maji katika Bwawa la JNHPP amesema kuwa, hadi kufikia Januari 16, 2023 kimo cha maji cha Bwawa kilifikia mita 112.48 kutoka usawa wa bahari kutokea kimo cha mita 74, Desemba 22, 2022. Naibu Waziri ameongeza kuwa, utekelezaji wa mradi wa JNHPP sasa unaenda sanjari na utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 kutoka eneo la mradi hadi Chalinze mkoani Pwani na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambapo kwa ujumla miradi hiyo inaendelea kutekelezwa kwa kasi.

Kuhusu malipo kwa mkandarasi wa mradi huo alisema kuwa, tayari Serikali imeshalipa asilimia 74.7 ya malipo hayo ambapo gharama za mradi huo ni shilingi trilioni 6.5.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula aliipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo ikiwemo hatua ya kuanza kujaza maji kwenye bwawa hilo.

Aidha amesisitiza mradi huo kuendelea kutekelezwa kwa kasi ili asilimia za utekelezaji zilizobaki zikamilike kwa wakati.

MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE



**Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula aliipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo ikiwemo hatua ya kuanza kujaza maji kwenye bwawa hilo.**





# ARAB CONTRACTORS

## Mjenzi mkuu Bwawa la Nyerere

*Kampuni ya JV Arab Contractors ambayo pia inajulikana kama Al Makawloon Al Arab ni kampuni ya ujenzi ya nchini Misri, ambayo kwa sasa ndio wajenzi wakuu wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa Bwawa la Nyerere (JNHPP)*

ARAB CONTRACTORS

KAMPUNI HIYO ILIINGIA MKATABA WA UJENZI WA BWAWA LA KUFUA UMEME LA MWALIMU NYERERE NA SERIKALI YA AWAMU YA TANO ILIYOKUWA CHINI YA HAYATI RAIS DKT. JOHN MAGUFULI MWAKA

**2018**





MOJA YA MRADI NCHINI MISRI ULIOJENGWA NA ARAB CONTRACTORS

MWANZILISHI WA KAMPUNI HIYO ILIYOASISIWA MWAKA 1955 YENYE MAKAO MAKUU YAKE CAIRO NI OSMAN AHMED OSMAN, TANGU KUASISIWA KWAKE HADI SASA IMEKUWA NA MAFANIKIO MAKUBWA KUTOKANA NA KUJENGA MAJENGO, MADARAJA, BARABARA, RELI ZA KAWAIDA NA ZA KISASA NA MABWAWA MBALIMBALI KATIKA MAENEO MENGI YA AFRIKA







*JV Arab Contractors hadi sasa inaendelea kukamilisha ujenzi wa mradi wa JNHPP*











KWA SASA KAMPUNI HIYO MBALI NA KUJENGA BWAWA LA JNHPP NCHINI TAZANIA PIA INAENDELEA NA MIRADI KADHAA NCHINI MISRI, LEBANON, UGANDA NA KUWAIT.

KAMPUNI ya JV Arab Contractors ambayo pia inajulikana kama Al Mokawloon Al Arab, ni kampuni ya ujenzi na kandarasi ya nchii Misri, ambayo kwa sasa ndio wajenzi wakuu wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa Bwawa la Nyerere (JNHPP) linalojengwa Rufiji, mkoani Pwani nchini Tanzania.

Mwanzilishi wa kampuni hiyo iliyoasisiwa mwaka 1955 yenye makao makuu yake Cairo ni Osman Ahmed Osman, tangu kuasisiwa kwake hadi sasa imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kujenga majengo, madaraja, barabara, reli za kawaida na za kisasa na mabwawa mbalimbali katika maeneo mengi ya Afrika. Kwa sasa kampuni hiyo inayomilikiwa na Serikali ya misri inakadiriwa kuwa na wafanyakazi 72,097.

**UJENZI WA JNHPP**

Kampuni hiyo iliingilia mkataba wa ujenzi wa bwawa la kufua Umeme la Mwalimu Nyerere na serikali ya awamu ya Tano iliyokuwa chini ya Hayati Rais Dkt. John Magufuli mwaka 2018. Thamani mkataba huo inakadiriwa kufikia dola za kimarekani bilioni 2.9 ambayo ni sawa na takribani shilingi trilion 6.5 za kitanzania.

JV Arab Contractors hadi sasa imefanikiwa kuukamilisha ujenzi wa mradi wa JNHPP kwa zaidi ya asilimia 60 na majaribio ya mradi huo unatarajia kuzalisha megawati 2115 za umeme yataanza kufanyika mapema mwaka 2024.

**MIRADI MINGINE**

Kwa sasa kampuni hiyo mbali na kujenga Bwawa la JNHPP nchini Tazania pia inaendelea na miradi kadhaa nchini Misri, Lebanon, Uganda na Kuwait.



**KWA SASA**

KAMPUNI HIYO INAYOMILIKIWA NA SERIKALI YA MISRI INAKADIRIWA KUWA NA WAFANYAKAZI

**72,097**

BAADHI YA MIRADI YA

# ARAB CONTRACTORS

Nchini Misri inaendesha miradi 14 baadhi yake ikiwa ni ujenzi wa jengo jipya la Bunge, Maghorofa marefu yam ji mpya wa El Alamein,ujenzi wa reli ya kisasa Kairo, barabara ya njia 12 ya Oases kwenye jiji wa 6 October. Miradi mengine ni ujenzi wa bwawa la Aswan, stesheni ya reli ya treni za kasi, nja ya Misri kampuni hiyo inajenga bandari nchini Lebanon, nchini Uganda kampuni hiyo inajenga barabara inayotoka Pallisa kwenda Masaka na nchini Kuwait kampuni hiyo inajenga mradi wa East Taimaa.










Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri "**Employer Portal**" na mwanachama "**Member Portal**" inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko "**www.nssf.or.tz**" bofya kifute cha "**Self Service**" (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa "**Employer Portal**" ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa "**Member Portal**" unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania

KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## JNHPP YAJAYO YANAFURAHISHA

MAENDELEO ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa maji katika bwawa la Julius Nyerere ni mazuri, hatua hiyo inaashiria wazi kuwa neema imeifikia Tanzania.

Tunaamini kukamilika kwa mradi huo ulioanza kujengwa wakati wa utawala wa serikali ya Awamu ya Tano, ambao utagharimu kiasi cha tsh 6.558 trilioni, kuna beba manufaa mengi kwa nchi.

Mradi huo utaliingiza Taifa kwenye orodha ya nchi chache za Afrika zenye uhakika wa asilimia 100 ya upatikanaji wa umeme wakati wote wa mwaka kama ilivyo kwa Misri, Algeria, Moroko na Tunisia.

Orodha hii ni kwa hisani ya SDG7 kwenye ripoti yake ya Maendeleo ya Nishati. Taasisi hii imejitolea kufuatilia maendeleo ya upatikanaji wa nishati kote Afrika na kwingineko, kama sehemu ya shabaha za Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu (SDG7).

Huo ni mpango shirikishi wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati (IEA), Idara ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa (UNSD), Benki ya Dunia na washirika wengine.

Jarida hili limebaini kuwa kwa sasa Tanzania haipo hata katika nchi 20 zenye uhakika wa umeme barani Afrika, ambapo imezidiwa hat ana Kenya ambayo imeorodheshwa kwenye nafasi ya tisa ikiwa na uhakika wa umeme kwa asilimia 70.

Ukiondoa Moroco, Misri, Algeria na Tunisia, nchi nyengine zilizoiacha Tanzania mbali kwenye upatikanaji wa umeme wa uhakika ni Gabon ambayo ina asilimia 91, Afrika Kusini 85%, Ghana: 84%, Botswana, 70%., Senegal: 70%, Libya 69%, Ivory Coast: 69% , Equatorial Guinea: 67% , Kameruni 63%, Nigeria: 55%, Namibia: 55%, Sudan: 54% , Eritrea: 50%, Ethiopia: 48% na Kongo: 48%.

Ukweli ni kwamba ukubwa wa Tanzania na wingi wa mito, maziwa na mabwawa iliyopo, haikupaswa kuwa nje ya nchi 20 bora zenye umeme wa uhakika, hata hivyo sisi tunaamini hatujachelewa.

Ujenzi wa Bwawa la Nyerere utatuondoa kwenye mkwamo huo na kutuweka kwenye kiwango cha juu cha nchi zenye umeme wa uhakika na ndio maana tunasema yajayo yanafurahisha.

Kukamilika kwa mradi huo na miradi mengine ya kuzalisha umeme wa gesi asilia kutaongeza zaidi ya Megawati 2,115 za umeme kwente gridi ya Taifa, aidha utaongeza wigo wa ajira viwandani na mashambani kwani wigo wa kuendesha kilimo cha umwagilia utapanuka mara dufu.

Rai yetu sisi TZ&BEYOND kwa watanzania wote ni kuhakikisha wanaulinda na kuuthamini mradi huo mkubwa ambao hakuna shaka yeyote umepewa nguvu kubwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameurithi kutoka kwa mtangulizi wake Hayati Rais Dkt. John Magufuli.

Aidha TZ&BEYOND tunapongeza awamu zote za uongozi kuanzia awamu ya kwanza iliyokuwa chini ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye ndie aliyezalisha wazo hilo.

Tunaamini kukamilika kwa mradi huo kutafungua milango mingi ya maendeleo na kusadifu kauli yetu ya yajayo yanafurahisha.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**



**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**


VISION PLUS EYE CLINIC

TIB CORPORATE BANK Your Partner Bank

KCB BANK

Air Tanzania The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK Tunakusikiliza

BOARD OF TRUSTEES NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND NSSF


# SHUKRANI

za dhati kwa WASHIRIKA WETU





# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

*The bank that listens*